OFISI YA RAIS TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

TAARIFA YA SIKU YA ELIMU – IDARA YA ELIMU SEKONDARI

1.1 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ni moja kati ya Halmashauri saba zilizopo katika Mkoa wa Mbeya. Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ina jumla ya Shule 31 za Sekondari kwa mchanganuo ufuatao:

- Shule 25 zinamilikiwa na Serikali ambapo Shule 22 zina Wanafunzi mpaka kidato cha nne, Shule mbili za kidato cha tano na shule 03 ni mpya ambazo ni (Busale,Njisi na Mwakilima).
- Shule 02 zinamilikiwa na Mashirika ya Dini.
- Shule 04 zinamilikiwa na watu/mashirika Binafsi..

2.0 HALI YA ELIMU SEKONDARI:

Kwa mwaka, 2021 Halmashauri ilikuwa na jumla ya wanafunzi **15,007** (wav **7,813** na was. **7,194**) wa kidato cha kwanza mpaka cha sita kwa Shule za Serikali, na Wanafunzi **1,076** wakiwemo (wav.**557** na was.**519**) kwa Shule zisizo za Serikali.

2.1: UANDIKISHAJI KIDATO CHA KWANZA 2021.

Mwaka 2021, jumla ya Wanafunzi **5,103** (wav.2540 na was. 2563) walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa Shule 22 za Serikali. Kwa mwaka 2022 Wanafunzi **5,461** (wav. 2665 na was.2796) wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza na kufanya kuwa na ongezeko la wanafunzi 358 ukilinganisha na mwaka 2021.

2.2: TAARIFA ZA WALIMU KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI

Kwa mwaka 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ilikuwa inahitaji walimu 694 wakiwemo walimu 251 wa masomo ya Hisabati na Sayansi kwa shule za sekondari za serikali. Hata hivyo bado kuna upungufu wa walimu 120 wa masomo ya hisabati ya sayansi sawa na asilimia **47.8.**

3.0 : HALI YA TAALUMA KWA SHULE ZA SEKONDARI.

Hali ya ufaulu katika Halmashauri ya Kyela ni nzuri na imekuwa ikipanda kila mwaka. Taarifa ya ufaulu kwa ujumla kwa miaka mitatu 2019 – 2021 ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

MTIHANI WA UPIMAJI KIDATO CHA PILI KWA MIAKA MITATU 2019 - 2021

NA.	MWAKA	Waliosajliwa kufanya Mtihani			Waliofanya Mtihani			Waliofaulu Mtihani			
		Wav	Was	Jumla	Wav	Was	Jumla	Wav	Was	Jumla	% ya Ufaulu
1	2019	1819	1816	3635	1715	1749	3464	1658	1693	3351	96.7378753
2	2020	2092	2144	4236	1963	2043	4006	1824	1940	3764	93.9590614
3	2021	2020	2276	4296	1857	2156	4013	1756	2085	3841	95.7139297

MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA NNE KWA MIAKA MITATU 2019 - 2021

NA.	MWAKA	Waliosajliwa kufanya Mtihani			Waliofanya Mtihani			Waliofaulu Mtihani			
		Wav	Was	Jumla	Wav	Was	Jumla	Wav	Was	Jumla	% ya Ufaulu
1	2019	1203	1307	2510	1381	1326	2707	1144	1075	2219	81.9726635
2	2020	1568	1458	3026	1535	1414	2949	1330	1320	2650	89.8609698
3	2021	1642	1615	3257	1604	1574	3178	1494	1397	2891	90.969163

MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA SITA KWA MIAKA MITATU 2019 - 2021

NA.	MWAKA	Waliosajliwa kufanya Mtihani			Waliofanya Mtihani			Waliofaulu Mtihani			
		Wav	Was	Jumla	Wav	Was	Jumla	Wav	Was	Jumla	% ya Ufaulu
1	2019	173	0	173	171	0	171	171	0	171	100
2	2020	254	0	254	254	0	254	246	0	246	96.8503937
3	2021	273	0	273	270	0	270	268	0	268	99.2592593

Ongezeko hili la ufaulu limewezekana baada ya kuunganisha nguvu na jitihada za wadau mbalimbali wa Elimu. Wadau hawa ni Serikali Kuu (Mdau Mkuu), Halmashauri yetu, Walimu,Wazazi na Wadau wengine wa elimu kama COCOA FOR SCHOOL na Taasisi za kifedha (CRDB BENKI na NMB BENKI) nk. Ushirikiano wa kila mmoja katika kutimiza wajibu ndio uliotufikisha hapo tulipo na safari bado inaendelea.

Katika kuendelea kufanikisha ongezeko hili la ufaulu Halmashauri inatoa zawadi kwa Walimu, Wanafunzi na Shule zilizoendelea kufanya vizuri kwa miaka mitatu mfululizo. Orodha ya Walimu, Wanafunzi na Shule zilizofanya vizuri imeambatanishwa na taarifa hii.

MIKAKATI YETU YA KUBORESHA ZAIDI UFAULU.

Kwa ujumla Idara imeweka mkakati wa kufanya ufuatiliaji wa karibu zaidi Shuleni ili kubaini mapungufu mbalimbali yanayoweza kufikisha ufaulu mzuri unaoendelea kujitokeza mwaka hadi mwaka. Baadhi ya mikakati mingine ambayo Idara inafanya ili ufaulu kwa vidato vya pili na nne ufikie 50% (Daraja la I – III) na kusiwe na daraja " O " ni pamoja na :

1. Kutembelea Shule zote kwa lengo la kuona ufundishaji na ujifunzaji ili kubaini mapungufu katika utekelezaji wa zoezi hili.
2. Kufanya vikao na Walimu ili kuwahamasisha na kujibu baadhi ya kero zinazowakabili zilizo ndani ya uwezo wa Halmashauri na kuzipeleka kwenye mamlaka za juu zilizo nje ya uwezo wa Halmashauri.
3. Kuongea na Wanafunzi wote na kuwakumbusha wajibu wao wawapo Shuleni na Nyumbani kwao wakati wa likizo kuzingatia masomo na kujisomea zaidi.
4. Kuhimiza Walimu kuwagawa Wanafunzi katika makundi kulingana na uelewa wao na kuwafundisha baada ya muda wa vipindi vya kawaida kwa kuzingatia kauli mbiu ya Halmashauri yetu ya " Kuondoa daraja la O " kwa kuhakikisha hakuna mwanafunzi anapata alama ya F masomo anayosoma.
5. Kuendeleza Mitihani ya pamoja kwa Shule zote za Halmashauri (Joint examination) katika mihula na mwisho wa mwaka ili kuleta uelewa wa pamoja na kuondoa tabia ya

uvivu miongoni wa Walimu. Hii ni pamoja na kushiriki mitihani ya utamihilifu (Mock examination) kwa madarasa ya mitihani.

6. Kuhimiza mahudhurio ya Walimu na Wanafunzi darasani na kuhakikisha hakuna Mwalimu au Mwanafunzi anayekosa vipindi darasani kwa sababu yoyote ile isiyo na msingi. Jukumu hili wanapewa zaidi Wakuu wa Shule kufuatilia kwa karibu.
7. Kuhimiza kufanyika kwa vikao vya Wazazi na Bodi za Shule ili kujadili maendeleo ya Taaluma Shuleni na kusogeza kwa karibu Ushiriki wa jamii katika kusimamia Taaluma Shuleni.
8. Kuhimiza mahusiano mema Shuleni na Jamii inayozunguka Shule kwa uongozi wa Shule kushiriki vikao vya " MABARAZA YA MAENDELEO YA KATA " (KAMAKA) kwa lengo la kutoa taarifa ya maendeleo ya taaluma ya Shule ndani ya Kata husika na tunashauri hii iwe ni moja ya agenda katika vikao hivyo.
9. Kuhimiza utaratibu mzuri kwa Wazazi wa Wanafunzi wote kupata chakula cha mchana ili baada ya hapo waweze kushiriki masomo ya muda wa ziada.
10. Kuhimiza shughuli za Michezo na Elimu ya kujitegemea kusimamiwa ipasavyo Shuleni bila kuingilia muda wa masomo. Hii itawaweka Wanafunzi vizuri kitaaluma na pia itasaidia Shule kutatua matatizo ya kiuchumi kwa kutegemea miradi yao wenyewe. Katika hili Shule zinahimizwa kuboresha viwanja vya michezo mbalimbali kadri uwezo wao wa kifedha unaporuhusu. Pia Shule zote zipande miti ya mbao, mapambo na vivuli pamoja na matunda ili kuinua uchumi wa Shule. Zoezi hili linaenda vizuri kwani hata Shule za mjini zimeshauriwa kuomba maeneo vijijini kwa ajili ya kupanda aina mbalimbali za miti.
11. Kusimamia na kuhakikisha Wanafunzi na Walimu wanazungumza "English"muda wote wawapo Shuleni ikiwa ni pamoja na kufundisha Program za kuimarisha uzungumzaji wa lugha hiyo ya kufundishia.
12. Kuzingatia ufundishaji wa "Baseline"ipasavyo na kutolea taarifa kwenye mamlaka husika.

CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIKAKATI.

1. Baadhi ya Wakuu wa Shule kushindwa kusimamia mikakati tajwa kutokana napengine kukaa zaidi ya miaka mitano katika kituo kimoja hivyo kuzoeleka sana na jumuiya ya Shule na jamii inayozunguka Shule . hii inawahusu pia walimu wa kawaida.
2. Tabia ya uvivu wa baadhi ya walimu katika kutekeleza majukumu ya Shuleni na hasa kama hawatasimamiwa ipasavyo na Wakuu wao wa Shule.
3. Utovu wa nidhamu na ukiukwaji wa maadili ya Ualimu kwa baadhi yao hupelekea taaluma Shuleni kushuka.
4. Mahusiano mabovu kati ya Shule , Wazazi na jamii inayozunguka Shule husababisha usiamamizi wa taaluma Shuleni kulegalega na hivyo kufifisha ufaulu ikiwa ni pamoja na kupelekea mahudhurio mabovu Shuleni.
5. Uhaba wa fedha na vitendea kazi unaoikabili Idara na Shule zetu na hivyo kushindwa kutekeleza baadhi ya mikakati tuliyojiwekea kama Idara ndani ya Halmashauri.

UTATUZI WA CHANGAMOTO:

1. Kuwabadilisha vituo vya kazi Wakuu wa Shule/Walimu waonaonekana kulegalega kama hatua ya awali ili wajirekebishe baada ya kubadili mazingira kabla ya hatua kali zaidi kuchukuliwa dhidi yao endapo hawatabadilika.
2. Tunaendelea kuwahamasisha Walimu kujitolea zaidi hasa muda wa ziada ili waweze kuwasaidia wanafunzi wenye uelewa mdogo. Zoezi hili linaendelea vizuri kwa Shule zote mwitikio ni mkubwa. Tunashauri pia jamii iunge mkono ili Walimu wajitolee zaidi pale inapowezekana.
3. Kuwachukulia Walimu hatua stahiki za kinidhamu na kisheria mara moja pindi inapobainika kwenda kinyume na Sheria na taratibu.
4. Kuhimiza kila Shule kuendeleza na EK (Elimu ya Kujitegemea) ili kujiongezea kipato. Aidha uongozi wa Shule unahimizwa kutumia fedha inayopatikana kutoka Serikalini kwa kufuata taratibu na miongozo ili kupunguza makali na uhaba wa fedha.

Naomba kuwasilisha.

IMEANDALIWA NA IDARA YA ELIMU SEKONDARI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA.

“MUNGU IBARIKI HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA”

KYELA BILA ZIRO INAWEZEKANA 2022.